

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 06 Amadou ma Amadou

Author: Ibrahima Ndiaye

LEARNING BY EAR 2010

SHALL I TELL YOU SOMETHING? AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE

EPISODE 06: „AMADOU MA AMADOU“

AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE

**EDITORS: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,
NAÏMA GUIRA**

TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS

PROOFREADING: TONY DUNHAM

KISUAHELI : ERIC PONDA

Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor

CHARACTERS:

1. NARRATOR (female, 40 years old, at least)
2. AMADOU (male, about 20 years old)
3. OLD WOMAN (female, sounding +/- 70 years old)
4. MORIBA (male, about 20 years old)

INTRO:

Hujambo na karibu kwa makala yetu ya sita ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga maisha yako, bado tukisalia katika Maada ile ile “JE NIKUDOKEZEE?” Hizi ni ngano za utamaduni wa Mwafrika kuhusu mbinu za kudumisha amani na maridhiano.

Kama ilivyo kawaida ngano ambazo huwasisimua wengi, vijana kwa wazee. Ni mbinu mahususi ya kuelezea picha halisi ya maisha ya mwanadamu na matukio duniani. Hivi leo tutasikia Ngano kuhusu kurejea kwa Mtoto mpotevu. Tega sikio ufahamu yaliyojiri katika hadithi hii ya “Amadou ma Amadou”.

1. MUSIC (*plays in background for the entire script*)

2. NARRATOR:

Hapo zamani za kale Mfalme mwenye hekima aliwahi kuitawala nchini ya Saraba. Nchi iliyojengwa kwa msingi wa kidini. Japo lilikuwa taifa dogo sana, lilibarikiwa ardhi yenye rotuba na kila mmoja aliishi kwa furaha. Mke wa mfalme alifuga mamba na kuzaa mtoto wa kiume aliyeitwa Amadou. Lakini maisha hayo ya furaha hayakudumu. Mfalme akiwa mawindoni alishambuliwa na chui na kufariki. Hata kabla ya kuzikwa, kila mmoja alifahamu fika kuwa, Amadou ndiye mrithi wa kiti hicho cha enzi. Siku chache tu majeshi yakioongozwa na sera za udikteta yalifanya mapinduzi. Hivyo Amadou akalazimika kukimbilia uhamishoni nje ya taifa hilo la Saraba. Alikasirika sana, lakini hakuwa na uwezo wa kufanya lolote kwani alikuwa mdogo sana. Miaka ilipita na Amadou akapendwa na wengi. Mwishowe akamuoa msichana mrembo sana kwa jina Fatima. Waliishi pamoja na kupata watoto. Familia yake iliishi kwa furaha na amani hadi baada ya mwaka mmoja ambapo nchi hiyo ilipokumbwa na ukame.

3. SFX: Wind blows over dry land

4. NARRATOR:

Baada ya miezi kadhaa ya ukame, chakula kikawa haba nchini humo. Amadou alihofia kumpoteza mkewe mpendwa na pia watoto wake. Hivyo akaamua kuhamia nchi nyingine kutafuta chakula cha kutosha kwa familia yake. Mbali na hayo, pia alikuwa na lengo moja la kudai ufalme wake. Lakini bila shaka, uamuzi wa kuondoka pia ulikuwa kama kuwasaliti wanawe waliomhitaji sana kwa malezi bora kama mzazi. Na kabla ya Amadou kuanza safari mkewe alimuahidi kwamba angewatunza watoto kwa muda wote atakapokuwa safarini.

5. COCK crowing

6. Narrator:

Siku iliyofuatia Amadou alianza safari yake asubuhi na mapema, akatembea mwendo mrefu, kuvuka mito, milima na mabonde, huku akipitia nchi ambazo hakuwahi kufika. Na baada ya muda, Amadou alishindwa kupata pesa za kutosha kumwezesha kurejea nyumbani. Lakini zaidi ni uchovu mbali na kukabiliwa na magonjwa kadhaa. Alijiona ana nuksi kwani kila alichofanya hakikufaulu. Siku moja alipokuwa akijipunzisha chini ya mbuyu huku akila chakula chake, alitafakari kuhusu maisha yake. Amadou hakuwa na hakika iwapo mipango yake ingemnyookea. Je, ndoto yake ilikuwa imegonga mwamba? Na kisha akashikwa na usingizi na kulala. Alipoamka, tayari jua lilikuwa linaeleka kutua, maana kwamba alilala mchana kutwa. Na bila ya kupoteza muda, aliamka na kuanza safari yake tena. Lakini njiani alikutana na Mwanamke ambaye alikuwa akijikokota barabarani, alionekana amedhoofika kutokana na ukosefu wa maji na chakula. Na hapo Amadou akaamua kumsaidia.

7. SFX: Quick footsteps on grass

8. Amadou:

“Mama, una shida gani ?Eh, kumetokea nini? Hebu ngoja nikusaidie. Twende pale chini ya ule mti mkubwa, kwani unahitaji kupumzika kidogo.”

9. Narrator:

Amadou akamchukua yule mwanamke hadi chini ya mti, akampa maji ya kunywa na chakula alichokuwa amebakisha. Na mara moja mwanamke huyo alichangamka na kumwambia Amadou:

10. Amadou: *drinking sounds*

11. Old woman:

“Kijana, umeniokoa sana! Ama kwa hakika umeokoa maisha yangu. Nilishambuliwa njiani na kunyang’anywa mali yangu yote! Lakini hebu niambie unafanya nini peke yako hapa?”

12. Amadou

“Kusema kweli ni hadithi ndefu sana Mama. Kama ujuavyo, maisha ni magumu. Nimeacha familia yangu kuja hapa kutafuta maisha bora, chakula cha familia yangu, lakini kama unavyoniona, nimeishia kuwa maskini zaidi kuliko nilivyokuwa hapo mbeleni.”

13. Old woman:

“Umenisaidia sana wangu na sasa ni zamu yangu kukusaidia. Nitakupa ushauri ambao daima unapasa kukumbuka: kamwe usijaribu kujiingiza katika hali usiyoweza kuimudu. Jaribu kufuata ushauri huo na ndoto yako itatimia.”

14. SFX: Footsteps of the old woman as she leaves

15. Narrator:

Na kisha Mama huyo akaondoka kumuacha Amadou bila ya kumfafanulia zaidi. Amadou alishangazwa na maneno na vituko vya mwanamke huyo. Alibaki akiwaza kwamba huenda mwanamke huyo alikuwa mwendawazimu. Na punde si punde kwa umbali akaona wingu la vumbi.

16. SFX: Galloping horses

17. Narrator:

Muda kidogo akawaona farasi kadhaa waliokuwa wakiongozwa na mtu aliyevalia mavazi ya mfalme akiwa juu ya farasi mmoja mweusi. Farasi wengine walikuwa wamebeba magunia yaliyojaa dhahabu na mapambo mengina ya vito. Ghafla mtu huyo akasimamisha farasi wake kando kidogo na Amadou na kisha akamuita.:

18. Moriba:

"Habari za jioni rafiki.!"

19. Amadou (*warily*)

"Ni njema sana !"

20. Moriba:

"Naitwa Moriba. Mimi ndie kitinda mimba wa kiume wa mfalme wa Saraba ambaye sasa ni marehemu. Lakini sikitiko langu ni kwamba babangu alikuwa habithi. Kakangu mkubwa alimrithi na sasa amekua katili kabisa. Nilirithi mali nyingi kama unavyoona hapa na nimeamua kuhama nchi hiyo na mali zangu zote kutafuta hifadhi mahali kwengineko."

21. Narrator:

Amadou alishangaa sana na hakuamini aliyokuwa akiambiwa na mambo anayojionea. Na hata hangeweza kukumbuka ufalme anakotoka Moriba.

22. Moriba:

“Hebu nisikilize hapa rafiki yangu, nitakupa sehemu ya mali hii ikiwa utanisaidia. Kwani kama unavyoona, utajiri huu wote ninaobeba ni hatari sana na naweza kuvamiwa na wezi wakati wowote.

Nakuomba uandamane nami kama mlinzi wangu endapo nitavamiwa. Na kutokana na msaada wako nitakulipa nusu ya mali yangu. Kusema kweli sijaona Mtu ninayeweza kumuamini kabisa, na ndio sababu nakuahidi nusu ya mali hii endapo utaweza kunisaidia.”

23. Narrator:

Amadou alikuwa akitetemeka kwa furaha kwani hakuamini aliyokuwa akiambiwa. Je, huu ndio uliokuwa upeo wa ndoto yake?

24. Amadou (*surprised, but lucky*)

“Ombi lako ni heshima kubwa sana kwangu Moriba. Na nakuahidi kuwa mwaminifu. Daima nitakuwa ubavuni mwako na hilo nakuhakikishia.”

25. Moriba:

“Basi panda farasi twende. Nafurahi kwamba umekubali ombi la kuandamana nami. Hebu panda yule farasi jike pale na kuanzia leo atakuwa wako.”

26. Narrator:

Amadou alipanda Farasi huku akitabasamu kwani kwa mara ya kwanza kabisa angeweza kuona mandhari ya nchi hiyo na hakuamini kabisa macho yake.

27. Amadou (to himself, joyful):

“Sasa nimepata rafiki na hivi karibuni nitakuwa tajiri na kurudi nyumbani kungana tena familia yangu.”

28. SFX: Galloping horses

29. Narrator:

Kwa muda wa majuma kadhaa wawili hao walijenga uhusiano na walifurahia kuwa pamoja. Amadou alijikakamua kumthibitishia rafiki yake kwambe yeye ni mlinzi wa kutegemewa.

Lakini siku moja walipokuwa wakisafiri, walifika kwenye mto mkubwa ambapo iliwabidi kufuata mkondo wa mto huo kutafuta sehemu isiyo na kina ili waweze kuvuka.

30. SFX: Torrential river

31. Moriba: “Amadou, hebu ingia kwenye mto utafute sehemu isiyokuwa na kina. Sitaki tupoteze mali yetu.”

32. Amadou Ndiyo, Moriba rafiki yangu..”

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 06 Amadou ma Amadou

Author: Ibrahima Ndiaye

33. Narrator:

Amadou hakuwa hodari wa kuogelea lakini alitaka kudhihirisha ujasiri wake na pia kama njia ya kutoa shukrani kwa Moriba. Na alipokuwa akijiandaa kujitosa mtoni, alikumbuka maneno yale aliyoambiwa na yule mwanamke aliyekutana naye barabarani; “Kamwe usijaribu kujiingiza katika hali usiyoweza kuimudu”.

Na hapo akasita kidogo na kisha akakiri mbele ya Moriba kwamba kamwe hajawahi kuogelea.

34. Moriba (*laughing*):

“Hahaha, mimi nilifikiri nimepata rafiki atakayeweza kunipa ulinzi kumbe ni mtu mwoga tu? Mimi ni tajiri mkubwa wa dhahabu lakini sasa nitalazimika kufanya mwenyewe kila kitu”

35. SFX: *Torrential river*

36. Narrator:

Hivyo Moriba akavua nguo zake na kujitosa mtoni. Aliweza kugusa ardhi chini ya mto huo huku akirajibu kuvuka hadi nga'mbo ya pili. Wakati tu Moriba alipomgeukia Amadou kumtaka avuke na farasi na mali yake, ghafla mamba akatokeza nyuma na kumshambulia. Amadou alishikwa na woga asijue la kufanya kumsaidia rafiki yake. Na baada ya mshtuko na huzuni ya kumpoteza rafiki yake, alianza kuwaza afanye nini. Sasa utajiri wote alikuwa ameachiwa. Na alikuwa na hiyari kutumia apendayo utajiri huo. Lakini je, hilo lilikuwa jambo la busara? Mara akakumbuka jina la ufalme wa Saraba lililotajiwa na Moriba! Hivi huyu alikuwa mtoto wa yule mfalme aliyetesa watu? Na hapo akaaamua kuurudisha utajiri huo kwa watu wa Saraba ambao wamenyanyaswa kwa muda mrefu na kupokonywa mali zao na mfalme huyo. Amadou aliwaongoza farasi hadi kijijini.

Alisafiri mchana kutwa hadi mji wa Malikunda, mji wa mfalme aliye mfahamu tangu utotoni. Mfale huyo Samory, alikuwa rafiki mkubwa wa marehemu Babake. Na alipofika katika makao yake, alipokelewa kwa furaha sana. Kisha Amadou akamueleza Mfalme Samory yote yaliyotokea na pia anayopanga kufanya.

37. Amadou:

"Hivi sasa naelekea Saraba nilikozaliwa. Nataka kuwarudishia wenyeji mali hii iliyoporwa kutoka kwao."

38. Narrator:

Samory alifurahishwa na hatua aliyoichukua Amadou. Mfalme Samory akamkaribisha Amadou kwenye kasri yake pamoja na mali aliyokuwa amebeba. Kutokana na uchovu wa safari ndefu, Amadou alipumzika kwa majuma kadhaa nyumbani kwa Mfalme. Kisha Mfalme Samory akakakubali kumsaidia Amadou na jeshi na ng'ombe wengi sana katika juhudi za kudai Ufalme wake wa Saraba.

39. SFX: *Sounds cattle, horses, soldiers walking*

40. Narrator:

Amadou alianza tena safari huku akiwa amezingirwa na jeshi kubwa na mifugo yake. Moja kwa moja walienda hadi mji mkuu wa Saraba, ambako habari za kurejea kwake zilisambaa kwa haraka na kuwafikia nduguze. Amadou alipendwa na wengi kutokana na umbo lake mbali na huruma zake kutaka kugawana na watu wa Saraba. Wakazi wa Saraba walimpokea kwa shangwe na kumkubali kama Mfalme wao. Na baadaye akawahutubia.

41. CROWD : Joyful cheering

42. Amadou

"Kwanza kabisa nataka kuwarudishia watu wangu mali yote iliyoporwa kutoka kwenu. Chukueni dhahabu zenu na mzitumie kwa manufaa ya jamii nzima!"

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 06 Amadou ma Amadou

Author: Ibrahima Ndiaye

43. CROWD : Joyful cheering

Akiwa bado mbele ya umma huo, Mfalme Amadou alizungumza na mwandani wake. Kisha akawamuru:

44. Amadou

“Nataka mniletee familia yangu hapa nyumbani kutoka uhamishoni. Mimi sitaki kabisa kuwa mbali tena na familia yangu sasa. Na pia mkamlete Mfalme Samory wa Malikunda, rafiki mkubwa sana wa Babangu. Nataka kumwalika kila mmoja kwa sherehe hii!”

45. CROWD: Crowd cheering, tam-tam, clapping hands

46. Narrator:

Baada ya miaka mingi, jimbo hilo la Saraba lilipata tena utajiri mkubwa na kuwa nchi ya amani kama ilivyokuwa awali. Amadou na familia yake waliishi pamoja kwa amani bila kutengana tena.

Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu.

47. MUSIC

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 06 Amadou ma Amadou

Author: Ibrahima Ndiaye

OUTRO:

Na hadi hapo msikilizaji ndipo tunafika mwisho wa makala hii ya sita ya ngano kuhusu Mfalme Amadou ma Amadou. Hadithi ya mtu aliyekata tamaa maishani baada ya kupoteza kila kitu. Lakini kwa sababu ya nia yake nzuri ya kutaka kuwasaidia wengine na kufuata ushauri na mawaidha, alipata tena utajiri huo na kuishi kwa amani. Je, umewahi kushuhudia kisa kama hiki? Tuandikie barua pepe kupitia anuani hii lbe@dw-world.de

Na iwapo unapenda kusikiliza tena makala hii au nyingine za Noa Bongo unaweza kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe.

Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.

END